



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA KONGWA

29, Machi 2022

TANGAZO LA KOTESHENI/HATI MSAKO

No. LGA/022/2021/2022/MFG/NC/01



KOTESHENI YA KUPATA MZABUNI WA KUVISHA MIFUGO HERENI (EAR TAGS)

1. Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa, ambapo kwa mujibu wa nukuu hii itajulikana pia kama Mwajiri inatarajia kuvisha mifugo hereni za utambuzi ambapo kila Ng'ombe/ Punda italipiwa Shilingi 1750/= na kila Mbuzi/Kondoo italipiwa Shilingi 1000/= ambapo gharama hizi zitalipwa na wafugaji wenyewe kwa mifugo yote ndani ya Halmashauri ya Kongwa. Mzabuni atakayepatikana atatakiwa kulipa shilingi mia moja kwa kila Ng'ombe/ Punda na Shilingi arobaini kwa kila Mbuzi/Kondoo atakayevishwa hereni.
2. Halmashauri inakaribisha wazabuni wenye sifa zilizotajwa katika kotesheni hii kuomba kazi ya kuvisha hereni mifugo.
3. Mwombaji atapewa nyaraka za kotesheni na hakutakuwa na ada ya zabuni katika ofisi ya Manunuzi ya Halmashauri ya Wilaya Kongwa.
4. Nyaraka za kotesheni zitapatikana katika ofisi ya Manunuzi ya Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa S.L.P.57, Ofisi ya Na. 17, Kuanzia saa 2:00 asubuhi hadi saa 9:30 alasiri, siku ya Jumanne tarehe 29/03/2022 hadi Ijumaa tarehe 01/04/2022 bila kujumuisha siku za mapumziko na sikukuu za Kitaifa.
5. Kotesheni irejeshwe ikiwa imefungwa katika bahasha, na ikiwa na nakala halisi (original copy), moja (1); na nakala kivuli (photocopy), moja (1)
6. Mwisho wa kupokea maombi ni Ijumaa ya tarehe 01 April 2022, saa 4:00 asubuhi, ikifuatiwa na ufunguzi utakaofanyika saa 4:30 asubuhi siku hiyo katika ukumbi wa Halmashauri. Waombaji/wawakilishi wanaweza kuhudhuria sherehe ya ufunguzi wa kotesheni hizo. Hivyo waombaji wanakaribishwa kuhudhuria ufunguzi.
7. Kotesheni zitakazorejeshwa kwa kuchelewa na zitakazotumwa kwa njia ya mitandao, kama vile nukushi na barua pepe hazitofunguliwa na hazitazingatiwa.
8. Bahasha ya nakala halisi (Original copy) na bahasha ya nakala kivuli (photocopy) zifungwe ndani ya bahasha moja na bahasha hiyo ifungwe madhubuti (sealed) na juu yake iandikwe anuani hii: Katibu wa Bodi ya Zabuni Wilaya, Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa, S.L.P. 57, Kongwa; kisha iandikwe jina la kazi iliyoombwa na namba yake.

Dr. Omary A. Nkullo
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
KONGWA

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
S. L. P. 57
KONGWA